## TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA JULAI HADI DESEMBA, 2020

### 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina utaratibu wa kutangaza taarifa za mapato ya ndani ya Halmashauri na matumizi ya mapato hayo kila robo mwaka ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri nchini. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI ameweka utaratibu wa kutoa taarifa hiyo kupitia Vyombo vya Habari. Taarifa hii ni ya robo ya pili ya mwaka wa fedha 2020/21 na hivyo imejumuisha taarifa ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri kuanzia Julai hadi Desemba, 2020.

Taarifa hii ina ainisha jinsi ambavyo vyanzo vikuu vinavyochangia katika mapato ya ndani ya Halmashauri na ufanisi wa kila Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani kwa kulinganisha makisio idhinishwa na mapato halisi (asilimia na wingi wa mapato ghafi). Uchambuzi wa matokeo umeandaliwa kwa kulinganisha aina za Halmashauri katika makundi na Kimkoa. Kadhalika, taarifa hii inaonesha mwenendo wa matumizi ya mapato hayo kwa kuainisha matumizi ya kawaida, matumizi ya miradi ya maendeleo ikiwemo asilimia kumi (10%) za mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

### 1.1 Hali ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Halmashauri zote

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri zilipanga kukusanya **Shilingi Bilioni 814.96** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Desemba, 2020 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 381.27** ambayo ni **asilimia 47** ya makisio ya mwaka. Itakumbukwa kwamba bajeti ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa iliongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 765.483** katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi **Shilingi Bilioni 814.96** katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Uchambuzi wa taarifa za mapato ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri katika kipindi cha Julai - Desemba, 2020 umeonesha kuwepo kwa ongezeko la mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 24.5** ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho cha Julai - Desemba, 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 7**. Aidha, katika kipindi hiki **Halmashauri ya Wilaya ya Momba** imeongeza jitihada katika ukusanyaji ukilinganisha na kipindi kilichopita cha mwaka wa fedha 2019/20 ambapo ilikuwa ni Halmashauri ya mwisho kwa asilimia ya makusanyo.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 Halmashauri **3** zimekusanya kati ya **asilimia 80 hadi asilimia 88** ambayo ni **asilimia 2** ya Halmashauri zote 185 na Halmashauri **73** zimekusanya kati ya **asilimia 50** hadi **asilimia 79** ya makisio ya mwaka ambayo ni **asilimia 39.** Aidha, Halmashauri **107** zimekusanya kati ya **asilimia 20** hadi **49** ambayo ni **asilimia 58** ya Halmshauri zote na Halmashauri **2** zimekusanya chini ya **asilimia 20** ya makisio ya mwaka.

Ufanisi wa Halmashauri katika kukusanya mapato ya ndani kwa ujumla wake katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020, **Halmashauri ya Wilaya ya Masasi** imeongoza kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 88** ya makisio yake ya mwaka na **Halmashauri za Wilaya za Kishapu** na **Longido** zimekua za mwisho kwa kukusanya chini ya **asilimia 20** ya makisio yake ya mwaka. *(Kiambatisho Na. 1A).*

Katika kuzipima Halmashauri zote kwa kigezo cha wingi wa mapato (pato ghafi), **Halmashauri ya Manispaa ya Ilala** imekusanya mapato mengi zaidi kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi Bilioni 30.67** na **Halmashauri ya Wilaya ya Itilima** imekusanya mapato kidogo kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi Milioni 324.89** *(Kiambatisho Na. 1B).*

## 1.2 Hali ya Ukusanyaji wa Vyanzo Vikuu vya Mapato ya Ndani

Vyanzo vikuu vya Mapato katika Halmashauri vinatambuliwa kutokana na asilimia ya uchangiaji wa kila chanzo katika jumla ya mapato yote ya ndani ya Halmashauri.

Kutokana na uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa mapato ya ndani katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Dec 2020 imabainika kuwa vyanzo Vikuu vya Mapato ya Halmashauri ni Ushuru wa Huduma (Service Levy), Ushuru wa Mazao (Produce cess), Ushuru wa Leseni za Biashara (Business licenses) na Mapato yatokanayo na Uchangiaji wa Huduma za Afya (User fee). Mchanganuo wa kila chanzo umeoneshwa katika Jedwali hapa chini.

**Jedwali 1: Mchanganuo wa mapato ya Vyanzo Vikuu vya Mapato ya ndani ya Halmashauri**

| S/N | CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO YA MWAKA (Billioni) | MAPATO HALISI (Bilioni) | ASILIMIA (%) YA UCHANGIAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Huduma | 141.82 | 75.03 | 20 |
| 2. | Ushuru wa Mazao | 110.02 | 68.14 | 18 |
| 5. | Uchangiaji wa Huduma za Afya | 106.48 | 38.62 | 10 |
| 4. | Leseni za Biashara | 51.70 | 24.17 | 6 |
| 5. | Vyanzo vingine | 404.94 | 175.31 | 46 |
| | **JUMLA KUU** | **814.96** | **381.27** | |

Katika jedwali hilo inaonesha kuwa chanzo cha Ushuru wa Huduma kina mchango mkubwa kwenye mapato ya Halmashauri kwa kuchangia **asilimia 20** ikifuatiwa na Ushuru wa Mazao **asilimia 18**, Uchangiaji wa Huduma za Afya **asilimia 10** na Leseni za Biashara **asilimia 6**. Aidha, chanzo cha **Uuzaji wa Viwanja** siyo chanzo cha kudumu ingawa katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 kimekusanya **Shilingi Bilioni 16.85** na kuchangia **asilimia 4** ya mapato yote. Vyanzo vingine vyote vimechangia asilimia chini ya tano hivyo, kuchukuliwa kama vyanzo vidogo ambavyo kwenye jedwali kwa ujumla vimechangia **asilimia 46.**

## 2.0 Uchambuzi wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri katika kipindi hiki umefanyika kwa kuzingatia aina za Halmashauri ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, uchambuzi huu umeainisha kiwango cha ukusanyaji wa mapato kwa kila Mkoa. Vigezo vilivyotumika katika kuoanisha Halmashauri na Mikoa ni Kigezo cha Asilimia ya mapato halisi na Kigezo cha Wingi wa mapato yaliyokusanywa.

### 2.1 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa Kuzingatia Asilimia ya Makusanyo

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Mkoa wa Katavi** umefanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo umekusanya wastani wa **asilimia 62** ya makisio ya mwaka ya Halmashauri za Mkoa huo. Aidha, Mkoa wa mwisho kwa kigezo hicho ni **Mkoa wa Simiyu** ambao umekusanya wastani wa **asilimia 36** ya makisio ya mwaka ya Halmashauri za Mkoa huo *(Kiambatisho Na. 2A).*

### 2.2 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Kimkoa kwa Kuzingatia Wingi wa Mapato

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Mkoa wa Dar es Salaam** umefanya vizuri kwa kigezo cha wingi wa mapato ambapo imekusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 89.13.** Mkoa wa mwisho katika wingi wa mapato ni **Mkoa wa Rukwa** ambao umekusanya **Shilingi Bilioni 4.07**. *(Kiambatisho Na. 2B).*

## 2.3 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa Kuzingatia Aina za Halmashauri kwa Kigezo cha Asilimia ya Makusanyo ikilinganishwa na Makisio ya mwaka

### 2.3.1 Halmashauri za Majiji

**Kundi hili linajumuisha Halmashauri 6**

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Halmashauri ya Jiji la Mwanza** imeongoza kundi la Halmashauri za Majiji kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 50** ya makisio yake ya mwaka na **Halmashauri ya Jiji la Dodoma** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya kwa **asilimia 39** ya makisio yake ya mwaka, *(Kiambatisho Na. 3A).*

### 2.3.2 Halmashauri za Manispaa

**Kundi hili linajumuisha Halmashauri 20**

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni** imeongoza kundi la Halmashauri za Manispaa ambayo imekusanya **asilimia 69** ya makisio yake. Katika kundi hili **Halmashauri ya Manispaa ya Singida** imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya kwa **asilimia 29** ya makisio yake ya mwaka. *(Kiambatisho Na. 3C).*

### 2.3.3 Halmashauri za Miji

**Kundi hili lina Halmashauri 22**

Katika kipindi nusu mwaka (Julai hadi Desemba, 2020) kwa kundi hilo la Halmashauri za Miji, **Halmashauri ya Mji wa Kahama** imeongoza kwa kukusanya kwa **asilimia 67** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambapo **Halmashauri ya Mji wa Bariadi** imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 23** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/*21 (Kiambatisho Na. 3E).*

### 2.3.4 Halmashauri za Wilaya

**Kundi hili lina Halmashauri 137**

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020, **Halmashauri ya Wilaya ya Masasi** imeongoza kwa kukusanya **asilimia 88** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, **Halmashauri za Wilaya za Kishapu na Longido** zimekuwa za mwisho katika kundi hilo kwa kukusanya chini ya **asilimia 20** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa Fedha 2020/21, *(Kiambatisho Na. 3G).*

## 2.4 Taarifa ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa Kuzingatia Aina za Halmashauri kwa Kigezo cha Wingi wa mapato.

### 2.4.2: Halmashauri za Majiji

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Halmashauri ya Jiji la Dodoma** imeongoza kundi la Halmashauri za Majiji kwa kigezo cha wingi wa mapato kwa kukusanya **Shilingi bilioni 18.53** na **Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi bilioni 5.66.** *(Kiambatisho Na. 3B).*

### 2.4.3: Halmashauri za Manispaa

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 kwa upande wa Halmashauri za Manispaa, **Manispaa ya Manispaa ya Ilala** imeongoza kwa kukusanya **Shilingi bilioni 30.70** na Halmashauri ya **Manispaa ya Kigoma/Ujiji** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 834.53,** *(Kiambatisho Na. 3D).*

### 2.4.4: Halmashauri za Miji

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 **Halmashauri ya Mji wa Geita** imeongoza kwa wingi wa Mapato katika Halmashauri za Miji ambapo imekusanya **Shilingi 5.60** na **Halmashauri ya Mji wa Mbulu** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 522.71,** *(Kiambatisho Na. 3F).*

### 2.4.5: Halmashauri za Wilaya

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2020 kwa kundi la Halmashauri ya Wilaya, **Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze** imeongoza kwa kukusanya mapato mengi ambapo imekusanya **Shilingi Bilioni 4.78**. Aidha, **Halmashauri ya Wilaya ya Itilima** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **Shilingi Milioni 324.89** *(Kiambatisho Na. 3H).*

## 3.0 Uchambuzi wa Matumizi ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 Halmashauri zimetumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 212.11** ambayo ni **asilimia 56** ya mapato halisi yaliyokusanywa. Kati ya matumizi hayo, **Shilingi Bilioni 113.05** zimetumika kwenye matumizi ya kawaida na **Shilingi Bilioni 99.10** zimetumika kwenye miradi ya maendeleo. Matumizi ya miradi ya maendeleo ni **asilimia 47** ya matumizi yote. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

| N/A | AINA YA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Matumizi ya kawaida (Recurrent expenditure) | 113,050,580,258.6 |
| 2. | Matumizi ya miradi ya maendeleo (Development Expenditure) | 99,060,992,909.83 |
| | **Jumla ya Matumizi hadi Desemba, 2020** | **212,111,573,168.43** |

### 3.1 Matumizi ya Mapato ya Ndani Katika Miradi ya Maendeleo

Uchambuzi wa taarifa za matumizi ya fedha za mapato ya ndani katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 unaonesha kuwa uchangiaji wa fedha za ndani katika shughuli za miradi ya maendeleo umezigawa Halmashauri katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni Halmashauri zinazochangia **asilimia 60** na kundi la pili ni Halmashauri zinazochangia **asilimia 40** ya mapato ya ndani. Kama ilivyoelezwa katika aya ya 3.0 fedha zilizotumika katika miradi ya maendeleo kwa kipindi hiki ni **Shilingi Bilioni 99.10**

Kundi la kwanza lina Halmashauri **169** ambazo zinatakiwa kuchangia **asilimia 40**, **Halmashauri ya Wilaya ya Njombe** imeongoza kwa kuchangia **asilimia 103** ya bajeti ya miradi ya maendeleo na Halmashauri za mwisho katika kundi hili ni **Halmashauri ya Mji wa Nanyamba** ambayo imechangia **asilimia 1 tu** ya bajeti ya miradi ya maendeleo. *(Kiambatisho Na. 4A).*

Kundi la pili lina Halmashauri **16** ambazo zinatakiwa kuchangia **asilimia 60** ya mapato ya ndani yasiyofungwa (own source proper) katika miradi ya maendeleo. **Halmashauri ya Mji wa Geita** imeongoza katika kundi hilo kwa kuchangia **asilimia 62** ya bajeti ya miradi ya maendeleo na **Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba** imekuwa ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 3** ya bajeti ya miradi ya maendeleo. *(Kiambatisho Na. 4B).*

## 3.2 Matumizi ya Mapato ya Ndani Katika Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Katika Kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020 Halmashauri zilitoa Mikopo kiasi cha **Shilingi Bilioni 22.33** kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni **asilimia 35** ya Bajeti ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambayo ni **Shilingi Bilioni 64.46**.

Uchambuzi wa taarifa unaonesha kuwa Halmashauri **14** zimechangia zaidi ya **asilimia 75** ya Bajeti ya mwaka ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Halmashauri **31** zimechangia kati ya **asilimia 50** hadi **74** ya bajeti ya mwaka ya mikopo hiyo na Halmashauri **87** zimechangia kati ya **asilimia 20 hadi 49** ya Bajeti ya mwaka ya mikopo hiyo. Aidha, Halmashauri **44** zimechangia **chini ya asilimia 20** na Halmashauri **9** hazijatoa kiasi chochote cha mkopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Katika kipindi hicho, Halmashauri iliyoongoza katika utoaji wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ni **Halmashauri ya Wilaya ya Musoma** ambayo imechangia **asilimia 107** ya bajeti ya mikopo hiyo na **Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti** imekua ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 4** ya bajeti ya mikopo hiyo na **Halmashauri 9 hazijatoa kiasi chochote cha mkopo** kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. *(Kiambatisho Na. 5).*

## 4.0 Changamoto za Ukusanyaji Mapato ya Ndani na Matumizi yake kwenye Halmashauri kwa Kipindi cha Julai hadi Desemba, 2020.

Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai, hadi Desemba, 2020 ni pamoja na zifuatazo:-

i. Baadhi ya Halmashauri kutegemea zaidi chanzo cha ushuru wa mazao na hivyo kushindwa kufikia malengo kutokana na kutokulipwa kwa wakati fedha za mapato ya chanzo cha ushuru wa mazao. Mfano; Ushuru wa zao la Pamba umeziathiri baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Simiyu na Shinyanga;

ii. Baadhi ya Halmashauri kujiwekea makisio kwenye vyanzo ambavyo hazina uhakika wa kukusanya. Changamoto hiyo imeziathiri baadhi ya Halmashauri ambazo zilikisia kukusanya mapato mengi kutoka katika chanzo cha kuuza Viwanja ambavyo havijauzika mfano Halmashauri ya Mji wa Bariadi.

iii. Baadhi ya Halmashauri hazisimamii kikamilifu matumizi ya mfumo ya kielektroniki ikiwemo matumizi ya Mashine za kukusanyia mapato (POS) na ucheleweshaji wa kupeleka fedha za mapato Benki;

iv. Kushindwa kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vipya vinavyobuniwa na Halmashauri;

v. Zipo Halmashauri ambazo hazisimamii kikamilifu matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na hivyo kusababisha kutopatikana kwa taarifa sahihi na kwa wakati;

vi. Bado zipo Halmashauri ambazo hazizingatii utaratibu wa kufanya usuluhishi wa mapato kwenye mifumo ya kielekitroniki kwa wakati. Mfano: **Halmashauri za Wilaya za Newala na Manyoni** ambazo zimechelewa kufanya usuluhisho wa mapato yake hadi tarehe ya kuandaa taarifa hii.

vii. Baadhi ya Halmashauri kuingiza fedha zisizo za vyanzo vya mapato ya ndani kwenye mfumo wa mapato ya ndani na hivyo kuonekana wamekusanya fedha nyingi ambazo sio sehemu ya Bajeti ya mapato ya ndani. Mfano: **Halmashauri ya Wilaya ya Longido** ambayo imeingiza kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.7** kwenye mfumo wa mapato ya ndani ikiwa ni fedha za fidia ya mradi wa Umeme wa REA kutoka TANESCO.

viii. Baadhi ya Halmashauri hazifuata kwa usahihi Mwongozo wa Matumizi ya Akaunti ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemevu na pia bado kuna Matumizi ya vifungu visivyo sahihi katika kufanya malipo ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemevu.

## 5.0 Mikakati ya Kutatua Changamoto

i. Upangaji wa Bajeti za Mapato ya ndani uzingatie uwezo halisi wa mapato ya kila chanzo (Revenue potential). Halmashauri zitumie takwimu sahihi katika kuandaa Makisio ya mapato ya ndani;

ii. Halmashauri ziongeze udhibiti wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya kielectroniki ili kuondoa mianya ya upotevu wa mapato;

iii. Mikoa inapaswa kuendelea kuzisimamia Halmashauri kutoa taarifa kupitia mifumo ya kielektroniki kwa kusisitiza kufanya usuluhishi wa taarifa katika mifumo mbalimbali na kusafisha takwimu chafu kwenye mfumo wa Epicor 10.2 ili kuwezesha kuwa na takwimu sahihi kwenye Dashboard ya mapato ya ndani;

iv. Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuandaa na kusimamia matumizi ya Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na kuendelea kusisitiza matumizi ya fedha hizo yaelekezwe kwenye vipaumbele vilivyomo kwenye mipango na Bajeti.

v. Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuzihimiza Halmashauri zote kufuata kwa usahihi Mwongozo wa Matumizi ya Akaunti ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemevu.

## 6.0 Hitimisho

Tunazipongeza Halmashauri zote zilizofanya vizuri katika kusimamia na kukusanya mapato ya ndani kwa kipindi hiki cha nusu mwaka (Julai – Desemba, 2020). Aidha, Mikoa ambayo Halmashauri zake zimekusanya mapato chini ya **asilimia 50** hazina budi kufanya tathmini na kuhakikisha zinaweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato katika vipindi vilivyosalia. Wakurugenzi wa Halmshauri ambazo hazijifikia **asilimia 50** ya makisio kwa kipindi hiki cha nusu mwaka wanatakiwa kujitathmini na kuweka mikakati mizuri ya kufikia malengo mwisho wa mwaka.

Tunaendelea kusisitiza kila Halmashauri kuendelea kutumia kwa usahihi mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na mifumo ya uhasibu ili kutoa taarifa kwa kufuata matakwa ya kisheria na kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS). Vilevile Mikoa iendelee kusimamia kwa karibu suala zima la ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri zilizopo katika Mikoa yao. Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kutangaza kwa umma taarifa za mapato ya ndani ya Halmashauri kila robo mwaka.

Selemani S. Jafo (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OR - TAMISEMI**